

## HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO

### MUHTASARI WA MKUTANO WA KAWAIDA WA MWAKA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA MANISPAA TAREHE 18/07/2019

#### Wajumbe waliohudhuria:

1. Mhe. Paschal M. Kihanga	—	Mstahiki Meya – Mwenyekiti
2. Ndg. John K. Mgalula	—	Mkurugenzi wa Manispaa - Katibu
3. Mhe. Sengo Isiaka Mtandikile	—	Naibu Meya - Mjumbe
4. Mhe. Amiri Juma Nondo	—	Mjumbe
5. Mhe. Dr. Christine Ishengoma (Mb)	—	Mjumbe
6. Mhe. Wenslaus Kalogeries	—	Mjumbe
7. Mhe. Zamoyoni Juma Abdallah	—	Mjumbe
8. Mhe. Amina H. Zihuye	—	Mjumbe
9. Mhe. Latifa Said Ganzel	—	Mjumbe
10. Mhe. Hadija Kombo Kibati	—	Mjumbe
11. Mhe. Dorothy J. Mwamsiku	—	Mjumbe
12. Mhe. Warda O. Bazia	—	Mjumbe
13. Mhe. Msasa Hamisi Mohamed	—	Mjumbe
14. Mhe. Rashid R. Mattesa	—	Mjumbe
15. Mhe. Daudi Salum Mnadi	—	Mjumbe
16. Mhe. Dismas Winfred Makanjira	—	Mjumbe
17. Mhe. Mizambwa R. Lugonzo	—	Mjumbe
18. Mhe. Kuruthum Isaack Mwisongo	—	Mjumbe
19. Mhe. Zahara S. Kitima	—	Mjumbe
20. Mhe. Ally Rashid Kalungwana	—	Mjumbe
21. Mhe. Zawadi Mohamed Kidando	—	Mjumbe
22. Mhe. Mudhihiri S. Shoo	—	Mjumbe
23. Mhe. Kifimbo Suddi Jumanne	—	Mjumbe
24. Mhe. Suzana Paulo Mtikwa	—	Mjumbe
25. Mhe. Zinduna Kombo Selemani	—	Mjumbe
26. Mhe. Castory Carlos Ndulu	—	Mjumbe
27. Mhe. Scolastica William Mkude	—	Mjumbe
28. Mhe. Hamisi A. Kilongo	—	Mjumbe
29. Mhe. Hilda Benedict John	—	Mjumbe
30. Mhe. Hassan Maringo	—	Mjumbe
31. Mhe. Peter Joel Dhahabu	—	Mjumbe
32. Mhe. Amini A. Tunda	—	Mjumbe
33. Mhe. Gabriel M. Temba	—	Mjumbe
34. Mhe. Spear A. Komanya	—	Mjumbe
35. Mhe. Mabula R. Lusewa	—	Mjumbe

36. Mhe. Gilbert Barnabas Mtafani	—	Mjumbe
37. Mhe. Bidiyanguze S. Madaraka	—	Mjumbe
38. Mhe. Samwel Msuya	—	Mjumbe
39. Mhe. Devotha Minja (Mb)	—	Mjumbe
40. Mhe. Juma Abdul Tembo	—	Mjumbe

### **Wajumbe wasiohudhuria kwa taarifa**

1. Mhe. Abdulazizi Mohamed (Mb)	—	Mjumbe
2. Mhe. Nuru Majikata	—	Mjumbe
3. Mhe. Milikiel Mansuet Mahiku	—	Mjumbe

### **Watendaji waliohudhuria**

1. Ndg. Waziri Kombo	—	Afisa Utumishi wa Manispaa
2. Ndg. Michael Waluse Joseph	—	Afisa Kilimo, Ushirika na Umwagiliaji wa Manispaa
3. Ndg. Etedy Mwanakatwe	—	Afisa Maendeleo na Ustawi wa Jamii wa Manispaa
4. Ndg. Wilfred W. Mramba	—	Mwanasheria wa Manispaa
5. Ndg. Nunkonge Kapula	—	Kny: Mkaguzi wa Ndani wa Manispaa
6. Ndg. Pendo S. Chagu	—	Afisa Uchaguzi wa Manispaa
7. Ndg. Upendo Elias	—	Mratibu wa Kudhibiti UKIMWI wa Manispaa
8. Ndg. Herman Njelekela	—	Kny: Afisa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano wa Manispaa
9. Ndg. Patrick E. Sijapenda	—	Afisa Usafirishaji wa Manispaa
10. Mhe. Dkt. Janeth Barongo	—	Afisa Elimu Sekondari wa Manispaa
11. Ndg. Rutaihwa John	—	Afisa Maendeleo ya Jamii
12. Ndg. Mariam Omary	—	Kny: Mhandisi wa Maji wa Manispaa
13. Ndg. Feliciano Katemana	—	Mratibu wa TASAF wa Manispaa
14. Ndg. Samwel Subi	—	Kaimu Afisa Mazingira na Udhibiti wa Taka ngumu wa Manispaa
15. Dr. Ikaji Z. Rashidi	—	Mganga Mkuu wa Afya wa Manispaa
16. Ndg. Elineema W. Mtaita	—	Katibu TSC wa Manispaa
17. Ndg. Abdul Buhety	—	Afisa Elimu Msingi wa manispaa
18. Ndg. Winfred A. Kipako	—	Afisa Tarafa wa Manispaa
19. Ndg. Mohamed M.O. Chamzhim	—	Afisa Mifugo na Uvuvi wa Manispaa
20. Ndg. Jacqueline Mushi	—	Kny: Mchumi wa Manispaa
21. Ndg. Safia Kagwahi	—	Afisa Utamaduni wa Manispaa
22. Ndg. Ruben Urassa	—	Mchumi
23. Ndg. Habibu Malengu	—	Kny: Afisa Manunuzi wa Manispaa
24. Ndg. Ponceano Kilumbi	—	Mweka Hazina wa Manispaa

25. Eng. Juma Gwisu \_\_\_\_\_ Kaimu Mhandisi wa ujenzi wa Manispaa  
26. Ndg. Barick Marandu \_\_\_\_\_ Mhasibu

**Sekretarieti:-**

1. Ndg. Lilian Henerico \_\_\_\_\_ Afisa Habari  
2. Ndg. Sylvia Kahitwa \_\_\_\_\_ Katibu wa Mikutano  
3. Ndg. Deogratias Butabile \_\_\_\_\_ Katibu wa Mikutano  
4. Ndg. Daudi Kibwana \_\_\_\_\_ Katibu wa Mikutano

HMM/BM/1/  
2019/2020  
Kufungua  
Mkutano

Kabla Mstahiki Meya hajafungua Mkutano, uliimbwa wimbo wa Taifa na Dua ya kuiombea Halmashauri.

Baada ya Dua, Mstahiki Meya alisoma hotuba ya utendaji kazi za Halmashauri zilizofanyika kwa Mwaka 2018/2019. Katika hotuba yake Mstahiki Meya alielezea kwa ufupi mafanikio yafuatayo:-

**1.0 MAPATO YA HALMASHAURI**

**Hali halisi ya makusanyo ya Mapato kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Juni, 2019.**

Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ilipokea na kukusanya fedha kwa mwaka 2018/2019 jumla ya **Tshs. 77,303,087,511.92** ambayo ni sawa na asilimia **107.76** ya makadirio ya **Tshs. 71,733,620,681.50** mwaka 2018/2019, kama ifuatavyo:-

- Mapato ya Ndani ya (Own Source) yalikuwa ni **Tshs. 5,270,626,176.39** ambayo ni sawa na asilimia **93.84** ya makisio ya **Tshs, 5,616,347,864.00** ya mwaka 2018/2019 kwa Mapato ya ndani.
- Miradi ya Maendeleo, jumla ya **Tshs. 18,525,457,642,39** ilipokelewa kutoka Serikali Kuu ambayo ni sawa na asilimia **104.01** ya makisio ya **Tshs. 17,811,251,433.50** ya mwaka 2018/2019.
- Mishahara, jumla ya **Tshs. 52,286,576,600.00** ilipokelewa ambayo ni sawa na asilimia **114.50** ya makisio ya **Tshs.45,666,511,344.00.**

**2.0 KUHUSU SEKTA YA UCHUMI NA UWEKEZAJI:**

Katika jitihada za kuongeza mapato ya Halmashauri, Manispaa ya Morogoro inashirikiana na Taasisi mbalimbali za fedha na Wadau katika ujenzi na uendelezaji wa majengo mbalimbali ya uwekezaji ambayo ni:-

- **Ujenzi wa Soko Kuu**

Halmashauri ya Manispaa Morogoro imeendelea na mpango wake wa ujenzi wa Soko Kuu jipya la kisasa katika eneo la Soko Kuu la zamani ambapo hadi sasa tumefika asilimia 52 ya ujenzi mradi mzima. Aidha kulingana na Mkataba Mkandarasi anapaswa kukabidhi kazi mwezi Septemba, 2019.

- **DDC**

Halmashauri imeshaandaa mpango wa biashara wa Kitega Uchumi cha Maendeleo ya Wilaya (DDC) ambapo gharama za ujenzi kulingana na usanifu majengo na BOQ ni takribani **Tshs. 620,000,000.00**. Hivyo Halmashauri imeandika barua ya kuomba mkopo kwenye Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa ili kuweza kujenga Kitega uchumi hicho.

- **Ujenzi wa Stendi ya Daladala.**

Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro inaendelea na ujenzi wa Stendi ya Daladala eneo la SUA Kata ya Mafiga, ambapo hadi sasa ujenzi kwa ajili ya Ofisi ya Mkandarasi unaendelea.

### **3.0 KUHUSU SEKTA YA MIUNDOMBINU:**

Kupitia Programu ya uboreshaji miji (ULGSP), chini ya mkopo wa Benki ya Dunia, shughuli zinazotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

#### **Barabara ya Barakuda kwa kiwango cha lami nzito (2.40 km).**

Ujenzi wa barabara ya Barakuda (2.40km) Mkandarasi anayejenga M/S G.N.M.S Contractors Company Ltd P.O. Box 107 Iringa atatumia kiasi cha **Tshs. 1,475,170,160.00**.

### **4.0 KUHUSU SEKTA YA ARDHI:**

Manispaa itaendelea kupima na kugawa viwanja ili kuweka mji katika mpangilio mzuri na kuboresha mazingira kwa kushirikiana na Benki ya Rasilimali Tanzania (Tanzania Investment Bank).

Manispaa imeandaa mpango mpya wa kusimamia ukuaji wa mji yaani Mpango Kabambe wa Manispaa ya Morogoro (The Morogoro Master Plan) 2016 – 2036 kwa kushirikiana na sekta binafsi na za umma. Aidha Halmashauri itaendelea kutekeleza mpango wa kuendeleza eneo la Biashara katikati ya Mji (Central Business District) ikiwa ni pamoja na mpango mkakati wa Maendeleo ya mji ( Strategic Urban Development Plan) 2008-2028.

Aidha, Manispaa imeingia ubia wa uendelezaji wa shamba la mkonge la Tungi kwa kushirikiana na wamiliki wa shamba hilo Dominion Plantations Limited ya Dar Es Salaam ili kujenga mji mpya wa Tungi (STAR CITY SATELITE TOWN). Mji huo mpya utawezesha Manispaa kufikia vigezo vya kuwa Jiji kutokana na huduma mbalimbali za viwanda, biashara, utalii, Bandari ya Nchi kavu na Hospitali ya Rufaa ya Kanda.

Shughuli za urasimishaji wa viwanja **9,921** kwa kutumia Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) katika mitaa mbalimbali ya Manispaa kwa kutumia wataalam waliopo na kwa kushirikisha sekta binafsi zinaendelea.

## **5.0 KUHUSU SEKTA YA ELIMU YA MSINGI:**

Halmashauri imefanikiwa kuongeza idadi ya wanafunzi walioandikishwa kuanza darasa la awali na darasa la kwanza.

### **Darasa la awali**

Wanafunzi waliosajiliwa kuingia darasa la Awali mwaka 2019 ni **4,885**, wavulana **2,554** na wasichana **2,331**.

### **Darasa la kwanza**

Wanafunzi waliosajiliwa kuingia darasa la kwanza mwaka 2019 ni **8,870** kati yao wavulana **4,371** na wasichana **4,499**.

### **Mafanikio ya Sekta ya Elimu Msingi:**

Kumekuwa na ongezeko la miundombinu ikiwemo madarasa, nyumba za walimu, matundu ya vyoo na samani katika shule za msingi kwa kiwango cha kuridhisha. Kwa mfano madarasa yaliyopo ni **656** na mahitaji ni madarasa **1,539** hadi Juni, 2019.

Aidha nyumba za walimu zilizopo ni **81** kati ya nyumba **1,978** zinazohitajika Juni, 2019. Pia matundu ya vyoo vya wanafunzi yaliyopo ni **681** ilipofika Juni 2019 na Madawati mahitaji ni **21,082** na yaliyopo ni **14,185** ilipofika Juni, 2019.

Kwa upande wa vitabu uwiano kwa wanafunzi umepungua toka **1:3** mwaka 2018 hadi **1:2** ilipofika Juni, 2019. Hali ya vitabu kwa sasa mashuleni kuanzia darasa la I – V inaridhisha. Halmashauri imepata vitabu kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

### **Mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi**

Waheshimiwa Madiwani Mwaka 2018 mtihani wa kumaliza elimu ya msingi ulifanyika mwezi Septemba, 2018. Jumla ya watahiniwa **7,296** walisajiliwa ambapo wavulana **3,566** na wasichana **3,730**.

Ufaulu wa wanafunzi waliomaliza darasa la saba mwaka 2018 ulikuwa ni **asilimia 88.74**, wanafunzi **6,431** walifaulu wakiwemo wavulana **3,096** na wasichana **3,335** kati ya **7,247** waliofanya mtihani wakiwemo wavulana **3,534** na wasichana **3,713**.

Aidha Halmashauri inaendelea kutekeleza agizo la Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kuhakikisha kuwa kusiwepo na mwanafunzi anayekaa chini kwa kukosa dawati. Halmashauri kupitia vyanzo vyake mbalimbali, Serikali Kuu na kushirikiana na wadau wanaendelea na uchongaji wa madawati kama jedwali lifuatalo linavyoonesha.

	<b>MAHITAJI</b>	<b>YALIYOPO</b>	<b>UPUNGUFU</b>
Awali	3,409	723	2,686
Msingi (I – VII)	20,570	14,477	6,093
<b>JUMLA</b>	<b>23,979</b>	<b>15,200</b>	<b>8,779</b>

#### **6.0 KUHUSU SEKTA YA ELIMU YA SEKONDARI.**

Halmashauri ina jumla ya shule **50**, kati ya hizo **23** ni za serikali na **27** ni za binafsi. Wanafunzi **28,551** wakiwemo wavulana **13,293** na wasichana **15,258**. Kati ya wanafunzi hao, wanafunzi **19,754** ni wa Shule za Sekondari za Serikali, wakiwemo wavulana **8,890** na wasichana **10,864**, na wanafunzi **8,797** ni wa shule za binafsi wakiwemo wavulana **4,403** na wasichana **4,394**.

#### **6.1 Watumishi wa Idara ya Elimu Sekondari**

Idara ya Elimu Sekondari ina jumla ya Walimu **1,155** wakiwemo wanaume **517** na wanawake **630**. Kati ya Walimu hao, Walimu **368** ni Walimu wa Sayansi na Hisabati ambao ni sawa na asilimia **38** na Walimu **787** ni wa masomo ya Sanaa. Aidha Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ina upungufu wa Walimu **35** wa masomo ya Hisabati na Sayansi. Pia ina ziada ya walimu **176** wa masomo ya Sanaa. Kuna jumla ya Watumishi wasio Walimu **26** wakiwemo wanaume **11** na wanawake **15**.

### **Miundombinu na Samani**

Idara ya Elimu ikishirikiana na Mhandisi wa Manispaa inasimamia ujenzi wa vyumba vya madarasa, ujenzi wa vyumba vya maabara za sayansi na samani.

#### **(a) Idadi ya Maabara na Hatua za Ujenzi**

MAHITAJI	ZILIZOKAMILIKA NA ZINATUMIKA	HATUA ZA UJENZI	
		UMALIZIAJI	ZILIZOEZEKWA
69	13	21	35

#### **(b) Miundombinu na Samani**

IDADI YA NYUMBA ZA WALIMU	IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA	MADAWATI		
		MAHITAJI	YALIYOPO	UPUNGUFU
60	328	19,754	14,982	4,772

### **Taaluma**

Ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha sita mwaka 2018 ni asilimia **99.6** hadi **99.7** mwaka 2018. Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha nne imeongezeka kutoka asilimia **69.9** mwaka 2016 hadi asilimia **84** mwaka 2018.

#### **7.0 KUHUSU SEKTA YA AFYA:**

- i) Halmashauri imeweza kununua mashine mbili za ultrasound na kuziweka katika vituo vya Afya Mafiga na Kingolwira.
- ii) Jengo la wodi ya wazazi katika kituo cha afya sabasaba
- iii) Ujenzi wa Placenta pits mbili katika zahanati ya mji mpya na mwembesongo.
- iv) Kuongezeka kwa idadi ya wajawazito wanaojifungulia katika vituo vya huduma kutoka asilimia 97 mwaka 2017/2018 hadi 99% mwaka 2018/2019.
- v) Vituo vya afya vilivyokuwa vinatoa huduma ya kupima wingi wa damu kwa wajawazito vimeongezeka kutoka 3 mwaka 2017/2018 hadi 19 mwaka 2018/2019.

- vi) Kuongezeka kwa huduma za uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi kutoka kituo kimoja mwaka 2017/2018 hadi viwili mwaka 2018/2019.
- vii) Kuongezeka kwa vituo vinavyotoa huduma kwa WAVIU (CTC) kutoka 11 mwaka 2017/2018 hadi 15 mwaka 2018/2019.
- viii) Kuanzishwa kwa chanjo ya kinga dhidi ya homa ya ini na saratani ya ini (hepatitis B vaccine) katika kituo cha afya saba saba.
- ix) Kuongezeka wigo huduma za macho kutoka kituo kimoja mwaka 2017/2018 hadi viwili 2018/2019.
- x) Idadi ya kaya zisizo na vyoo imepungua kutoka 14 mwaka 2017/2018 hadi zero 2018/2019.
- xi) Idadi ya kaya zenye vyoo bora imeongezeka kutoka kaya 69,744 (89%) mwaka 2017/2018 hadi kaya 72,033 (92%) mwaka 2018/2019.
- xii) Kubadili mfumo wa malipo ya uchangiaji (cost sharing) kutoka kulipa kiwango kimoja kwa huduma zote kwenda kwenye malipo ya huduma moja moja kadiri unavyotumia huduma. Hii itaongeza ufanisi wa vituo kwenye kuwahudumia wateja.
- xiii) Wigo wa dawa zinazopatikana vituoni umeongezeka, vituo vinavyotoa dawa za chanjo ya kichaa cha mbwa zimeongezeka kutoka kimoja mwaka 2017/2018 hadi viwili mwaka 2018/2019 (Mwembesongo na Uhuru), dawa za sukari shinikizo la damu zimeongezwa kwenye vituo vya afya.
- xiv) Huduma za meno zimeboreshwa kutoka kung'oa meno pekee mwaka 2017/2018 hadi kuziba meno mwaka 2018/2019.
- xv) Ukarabati wa kituo cha Afya Kingolwira unaendelea katika mwaka wa fedha 2018/2019.
- xvi) Mashine za maabara zimefanyiwa matengenezo katika vituo vya Afya Kingolwira na Sabasaba mwaka 2018/2019 ambapo wigo wa vipimo utaongezeka.
- xvii) Vituo vya huduma vimeongezeka kutoka 61 mwaka 2017/2018 hadi 64 mwaka 2018/2019.



## **8.0 SEKTA YA MAZINGIRA NA UDHIBITI WA TAKA NGUMU**

Shughuli za usafi wa mazingira kuzuia uchafuzi, utunzaji na upendezeshaji wa mazingira katika kipindi cha mwaka 2018/2019 zimeendelea kuboreshwa kwa Manispaa kufanya mambo yafuatayo:-

- i) Kuandaa na kuusambaza mwongozo wa usimamizi wa shughuli za usafi, kuzuia uharibifu, uchafuzi, utunzaji na upendezeshaji wa mazingira ngazi ya Kata na Mitaa.
- ii) Kata 24 kuingia mikataba ya kufanya usafi wa mazingira na vikundi vya usafi 63.
- iii) Kuinua kiwango cha uzoaji wa taka toka asilimia 71 hadi 79 ya taka zinazozalishwa kila siku.
- iv) Kupendezesha mazingira ya Manispaa kwa kutunza Bustani, kupanda miti na kuhamasisha wananchi kuanzisha vitalu vya miche ya maua miti, majani na kupanda maua na miti katika maeneo yanayostahili.
- v) Kufanya ukaguzi na kutoa elimu ya mazingira kwa Kata 11 zenye shughuli za uharibifu wa Mazingira.
- vi) Kusimamia agizo la Serikali la kuzuia matumizi ya mifuko ya plastiki.
- vii) Kutoa elimu ya usafi wa mazingira na kusimamia usafi wa kila siku na wa Jumamosi ya mwisho wa mwezi.

## **9.0 KUHUSU SEKTA YA MAJI:**

Manispaa ya Morogoro ina jumla ya Mitaa **69** ambayo ipo pembezoni mwa Mji. Mitaa hiyo haijafikiwa na mtandao wa bomba la maji safi na salama kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka (MORUWASA). Kuanzia mwaka 2007/2008 Manispaa ya Morogoro ilianza kutoa huduma ya Maji safi na salama katika Mitaa tajwa hapo juu kwa awamu. Mpaka Juni 2019 jumla ya miradi **13** imetekelezwa katika Mitaa ya **21** ambayo ni Mgambazi, Folkland, Kiswanya, Minazini, Tindigo, Nyambuwa, Bigwa Barabarani na Lukuyu, Lugala, Visole, Kibwe, Kiegea A, Mkoya, Kasanga, Misongeni A, Misongeni B, Tanki la Maji, Bomba la Zambia, Kigea B, Mundu na Kilala.

### **9.1 Lengo la Manispaa katika usambazaji wa Maji:**

Mwaka wa fedha 2018/2019 Manispaa ilikuwa na mpango wa kutekeleza miradi 3 ya maji ambayo ni:

- i) Ukamilishaji wa mradi wa maji – Mundu na Kilala
- ii) Mradi wa maji wa Kata ya Magadu na Mindu
- iii) Mradi wa maji wa Mtaa wa Kipera

Hadi kufikia Juni, 2019 hali ya utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

#### **i) Mradi wa Maji wa Mtaa wa Mundu na Kilala**

Mradi umeanza kujengwa tarehe 01.05.2018

##### **Kazi zilizopangwa kufanyika**

- Ujenzi wa banio la maji
- Ujenzi wa Tanki la maji lenye ujazo wa meta za mraba 100
- Ujenzi wa vituo 14 vya kutolea maji
- Ujenzi wa laini kuu ya bomba la kupeleka maji kwenye tenki
- Ujenzi wa laini kuu na ndogo ya kusambazia maji kwenye vituo

##### **Hali ya utekelezaji**

- Ujenzi wa laini kuu ya kupeleka maji kwenye tanki umekamilika
- Ujenzi wa laini kuu na ndogo za kusambaza maji kwenye vituo umekamilika
- Ujenzi wa tenki kuu umekamilika kwa asilimia 90
- Ujenzi wa vituo vya kuchotea maji umekamilika
- Ujenzi wa banio umekamilika kwa asilimia 90.
- Mradi umefikia asilimia 95 ya utekelezaji.

#### **ii) Mradi wa maji wa Kipera**

Uchimbaji wa kisima kirefu kimoja (mita 100) ulifanyika Mtaa wa Ngerengere na maji mengi yalipatikana, baada ya kufanya vipimo vya maji yaliyopatikana ilibainika maji yana chumvi nyingi iliyozidi viwango vya kitaifa vinavyotakiwa kutumiwa kwa matumizi ya majumbani. Hivyo iliamuliwa kisima hicho kifukiwe. Kwa sasa Halmashauli inaendelea kuwasiliana na MORUWASA ili kuangalia uwezekano wa kupeleka maji ya mtandao wa mabomba ya MORUWASA.

**iii) Mradi wa maji wa Kata ya Magadu na Mindu**

Usanifu wa mradi ulifanyika na kukamilika kwa kutegemea kutumia chanzo cha maji cha mto Mlali, Manispaa iliomba kibali cha kutumia maji ya mto mlali kutoka Bodi ya Bonde la Wami/Ruvu kuwa chanzo hakitoshelezi kwa kuhudumia mahitaji ya watu 13,000 labda watoe kibali kwa matumizi ya miezi miwili tu ya Aprili na Mei, kwani chanzo hicho kinatumiwa na MORUWASA na wamepatiwa kibali.

Kwa sasa usanifu unaendelea kufanyika kwa ushirikiano wa Ofisi ya Mkoa, Manispaa, MORUWASA na Bodi ya Bonde la Wami/Ruvu kwa kutumia chanzo cha maji cha mto Tangeni.

Taratibu za manunuzi za mradi wa maji wa Kata ya Mindu zimekamilika na mkataba umewasilishwa Wizara ya Maji kuomba kupatiwa kibali cha kuingia mkataba na mkandarasi aliyepatikana.

**iv) Wadau wa maendeleo**

Aidha katika kipindi cha Julai 2018 hadi Juni 2019 Manispaa ya Manispaa ya Morogoro kwa kushirikiana na mdau wa maendeleo Shirika la Islamic Foundation imefanikiwa kuchimba visima virefu 2 katika maeneo yafuatayo, Shule ya Sekondari ya Morogoro na Shule ya Sekondari Nanenane.

**9.2 Kuanza kazi kwa wakala wa usambazaji maji na usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA)**

Manispaa ya Morogoro imepokea maelekezo kutoka Wizara ya Maji, kuelezea uanzishwaji wa Sheria Na. 5 ya mwaka 2019 ya huduma za maji na usafi wa mazingira inachukua nafasi ya Sheria Na. 12 ya mwaka 2009. Sheria tajwa hapo juu imeanzisha Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Rural Water Supply and Sanitation Agency – RUWASA). Wakala huu utakuwa na jukumu la kusimamia Sekta ya Maji Vijijini, ikiwemo ujenzi wa miradi ya maji na utolewaji wa huduma ya maji.

Kwa mujibu wa notisi iliyotolewa na Wizara ya Maji Sheria mpya inaanza kutumika rasmi kuanzia tarehe 1, Julai 2019.

**10. Utawala Bora.**

Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ilifanya ziara ya mafunzo katika Halmashauri ya Jiji la Tanga tarehe 17-18/12/2018 na Kamati ya Fedha na Uongozi ilifanya ziara katika Manispaa ya Mtwara Mikindani tarehe 19-

21/06/2019 kubadilishana ujuzi na maarifa katika nyanja za ukusanyaji mapato ya ndani, utambuzi wa fursa, uibuaji na usimamizi wa miradi ya maendeleo, utunzaji wa mazingira, Sheria Ndogo na matumizi yake.

Aidha nasi tulipokea wageni waliokuja hapa kufanya ziara ya mafunzo, zikiwemo Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Paul Makonda, Waheshimiwa Madiwani wa Kamati ya Maadili wa Manispaa ya Temeke na Halmashauri Wilaya ya Geita ambapo Halmashauri zote zilibadilishana uzoefu.

## **11. 0 MAPAMBANO DHIDI YA VVU NA UKIMWI**

Kwa kuzingatia ujumbe wa mapambano dhidi ya UKIMWI wenye kauli mbiu '*Tanzania bila maambukizi mapya, unyanyapaa na vifo vitokanavyo na UKIMWI inawezekana*' Halmashauri ina idadi ya vituo vinavyotoa huduma ya upimaji **50**. Kwa kipindi cha mwaka 2018 kiwango cha maambukizi ni **asilimia 4.9**. Watu walio kwenye matumizi ya dawa za kupunguza makali ya UKIMWI (ARV) kwa sasa (Current on ART) ni wanaume **3,137** na wanawake **8,734** jumla **11,871**.

Idadi ya watu waliopima mwaka 2018 ilikuwa wanaume **35,690** na wanawake **55,608** jumla **92,328**. Waliokutwa na maambukizi ni wanaume **1,495** na wanawake **3,119** jumla **4,614**.

### **11.1 Mikakati ya kupunguza maambukizi mapya ya VVU kwa mwaka 2015 hadi 2020 - (90, 90, 90)**

- **90** – Asilimia tisini ya jamii wawe wanajua hali ya maambukizi kwa kupitia upimaji wa VVU.
- **90** – Asilimia tisini ya watu wote waliopima wataanzishiwa dawa za (ARV) za kufubaza ukali wa virusi vya UKIMWI.
- **90** – Asilimia tisini ya watu wote wanaotumia ARV kiwango cha Virusi vya UKIMWI kinapungua kwa kiasi kikubwa.
- Kushirikiana na wadau mbalimbali wanaojishughulisha na mapambano ya VVU na UKIMWI.
- Kuhakikisha kuwa Konga ya watu wanaoishi na VVU Manispaa ya Morogoro inaendelea kupatiwa Elimu ya kuweza kuwashawishi wenzao kupima na kufanya shughuli mbalimbali za ujasiliamali.

## **12.0 SEKTA YA KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 sekta ya kilimo, Umwagiliaji na Ushirika imetekeleza shughuli zifuatazo;

- Kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa bei elekezi ya kuuzia mbolea ya kupandia aina ya DAP na mbolea ya kukuzia aina ya UREA zinazotolewa na mamlaka ya Udhambi wa Mbolea Tanzania (TFRA) ambapo wakulima **4,727** kwenye Kata **29** walielimishwa. Mbolea ya kupandia (DAP) iliuzwa kwa shilingi **62,346.00** na mbolea ya kukuzia (UREA) iliuzwa shilingi **54,006.00** kwa mfuko wa kilo **50**.
- Kufanya maandalizi ya awali ya sikukuu ya wakulima Nanenane 2018 kwa kupanda mbegu za aina mbalimbali pamoja na kutunza vipando vya kudumu na vya muda mrefu, kununua vifaa mbalimbali kwa thamani ya shilingi **6,000,100.00**.
- Kutoa ushauri wa mbinu bora za uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kwa Wakulima **7,735** kwa kuzingatia kalenda ya msimu wa kilimo.
- Kusimamia mashamba Darasa ya kilimo bora cha migomba kwa kushirikiana na sekta binafsi.
- Idadi ya vyama vya ushirika iliongezeka kutoka **159** ya mwaka 2018 hadi **165** kwa mwaka 2019.

## **13.0 SEKTA YA MIFUGO**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha **2018/2019** sekta ya Mifugo na Uvuvi imetekeleza shughuli zifuatazo:-

- **Ufugaji bora**

Jumla ya wafugaji **16,008** (wafugaji wa kuku **6,612** na wafugaji wa ng'ombe na mifugo mingine **9,396**) kutoka kata mbalimbali za Manispaa ya Morogoro walipatiwa mafunzo ya kanuni bora za ufugaji.

- **Usindikaji**

Jumla ya wadau **208** walipatiwa elimu ya Maziwa ikiwa ni pamoja na, utunzaji na uhifadhi bora wa maziwa, usafirishaji mzuri wa maziwa na usindikaji wa maziwa.

- **Uboreshaji wa Koosafu**

Katika kutimiza lengo la kuboresha koosafu za Ng'ombe wa maziwa na kuongeza tija ya uzalishaji wa maziwa, Halmashauri ya Manispaa ya

Morogoro ilitoa mafunzo ya Uhimilishaji (Artificial insemination) kwa jumla ya wafugaji **5,016** kutoka kata zote za Manispaa ya Morogoro. Aidha hadi sasa jumla ya Ng'ombe **1,080** wamehimilishwa.

- **Uzalishaji na hifadhi ya malisho**

Mafunzo ya uzalishaji wa malisho ya mifugo yalifanyika kwa wadau **3,301** Kutoka sehemu mbalimbali za Manispaa ya Morogoro.

### **13.1 Ufugaji wa Samaki katika Mabwawa.**

Mafunzo ya ufugaji wa samaki yalitolewa kwa wadau **2,400** Kutoka maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Morogoro.

Aidha jumla ya mabwawa ya kufugia samaki **147** yalianzishwa na watu binafsi katika maeneo mbalimbali kama vile Mzinga, Mkundi, Mazimbu, Bigwa, Kihonda nk.

### **Utoaji wa Chanjo kwa Mifugo**

<b>NA</b>	<b>Aina ya Mifugo</b>	<b>Idadi ya Mifugo iliyochanjwa</b>	<b>Ugonjwa</b>
1	Ng'ombe	1,492	CBPP
2	Ng'ombe	745	ECF
3	Ng'ombe	2,983	ATHRAX
4	Ng'ombe	961	NDOROBO
5	Mbuzi	1,826	CCPP
6	Mbwa	659	RABIES
7	Mbwa	101	DHLP
8	Paka	93	RABIES
9	Kuku	1,509,345	MDONDE
10	Kuku	1,233,927	GUMBORO
11	Kuku	386,034	NDUI

Kuhusu mbwa wazururaji, Idara imeendelea kutumia mitego **2** ambayo ilitengenezwa kwa ajili ya kukamatia mbwa wanaozurura ili kudhibiti mbwa hao. Jumla ya mbwa **97** wamekamatwa kwa kutumia mitego hiyo.

### **14. 0 SEKTA YA MAENDELEO, USTAWI WA JAMII NA VIJANA**

Vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu vimepatiwa elimu ya ujasiriamali na kupewa mkopo unaotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri. Kwa sasa mkopo unaotolewa hauna riba ambapo

**asilimia 4** ni kwa vikundi vya wanawake, **asilimia 4** kwa vikundi vya vijana na **asilimia 2** kwa vikundi vya watu wenye ulemavu. Lengo la kuwapatia mkopo ni kuongeza mtaji katika biashara zao ambazo tayari wamezianzisha ili waweze kuzalisha kwa wingi na hatimaye kujikwamua kiuchumi na kuondokana na umaskini katika familia zao.

Kwa kipindi cha mwaka 2018/2019 jumla ya vikundi **50** vya wanawake vimepatiwa mkopo wenye thamani ya shilingi **128,500,000.00**, Vikundi vya vijana **36** vimepatiwa mkopo wenye thamani ya shilingi **89,500,000.00** na vikundi **11** vya watu wenye ulemavu wamepatiwa mkopo wenye thamani ya shilingi **30,500,000.00**. Hivyo jumla ya shilingi **248,500,000.00** zimekopeshwa kwa vikundi hivyo.

Jamii imejengewa uwezo wa juu kuhusu uundaji vikundi na kuvisajili ambapo hadi sasa jumla ya vikundi **231** vimesajiliwa na wameweza kufungua akaunti katika benki na kujiwekea akiba.

#### **14.1 Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

Jukwaa la uwezeshaji wanawake kiuchumi limewezeshwa kupata vyereheni **17** na mashine za overlock **2** kwa gharama ya **Tshs. 5,000,000.00** kutoka Mfuko wa Jimbo. Vyerehani hivi vilipatikana baada ya uzinduzi wa Majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi katika Kata zote **29** za Manispaa ya Morogoro. Vyerehani hivi vitatumika kufungua darasa la ushonaji.

#### **15.0 MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI (TASAF III)**

Manispaa ya Morogoro ni miongoni mwa Halmashauri **161** zinazotekeleza TASAF awamu ya tatu kupitia Mpango wa kunusuru kaya maskini, wenye Malengo ya kuwezesha kaya maskini kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu.

Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ina jumla ya Walengwa **2,850** mpaka kufikia Juni, 2019 toka katika Mitaa **164** toka katika kata zote **29** inayotekeleza mpango wa kunusuru kaya maskini (TASAF III ).

#### **15.1 Uhawilishaji Fedha kwa Kaya Maskini**

##### **Mafanikio:-**

- Kupitia Mpango wa TASAF kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 Manispaa ya Morogoro ilipokea jumla ya shilingi **378,525,730.00** toka TASAF makao makuu na kufanya uhawilishaji kwa Walengwa wa kaya Maskini **2,850**.

- Walengwa wa Mpango wameweza kukuza kipato cha familia na kuwa na uwezo wa kupata milo mitatu kwa siku Walengwa **1,276** waliotembelewa walithibitisha
- Walengwa **79** toka mitaa mbalimbali ya mpango walihojiwa kupitia ruzuku wameweza kupata fedha ambazo zinawasaidia kulima mashamba ya mahindi na Alizeti
- Kupitia ruzuku hii kuna walengwa takriban **1312** sawa na asilimia **46.04** wameweza kuanzisha biashara ndogo ndogo za kuuza ndizi, magenge, ufugaji wa mifugo kama mbuzi, nguruwe n.k.
- Walengwa pia wameweza kujiwekea akiba kwa ajili ya kuhudumia matibabu ya familia yao kwa kujiunga na mfuko wa afya ya jamii (CHF) baada ya uhamasishaji. Jumla ya Kaya **874** zimejiunga na CHF.
- Kuongezeka kwa uwezo wa kuhudumia mahitaji ya shule kwa watoto wao kama madaftari, sare za shule na mahitaji mengine ya msingi

Baada ya hotuba hiyo Mstahiki Meya alifungua Mkutano saa 7:40 mchana.

HMM/BM/2/  
2019/2020  
Kuridhia  
agenda za  
Mkutano

Baraza la Madiwani liliridhia agenda zifuatazo:-

1. Kufungua Mkutano
2. Uchaguzi wa Naibu Meya wa Halmashauri kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2019/2020.
3. Kuteua Wajumbe wa Kamati za kudumu za Halmashauri kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.
4. Kupitisha Ratiba ya Mikutano ya Halmashauri na vikao vya Kamati za kudumu kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.
5. Taarifa ya utendaji kazi za Halmashauri kwa mwaka 2018/2019
6. Kufunga Mkutano

HMM/BM/3/  
2019/2020  
Uchaguzi wa  
Naibu Meya  
wa  
Halmashauri  
kwa mwaka  
wa fedha  
2019/2020

Mkurugenzi wa Manispaa (Katibu) alitoa taarifa kuwa alipokea barua kutoka Chama Cha Mapinduzi Wilaya (CCM) ikimtambulisha Mheshimiwa Sengo Isiaka Mtandikile kuwa mgombea wa nafasi ya Naibu Meya wa Halmashauri kwa mwaka 2019/2020 na barua kutoka Chama Cha Demokrasia na Maendeleo Wilaya (CHADEMA) ikimtambulisha Mheshimiwa Scolastica W. Mkude kuwa mgombea wa nafasi ya Naibu Meya wa Halmashauri kwa mwaka 2019/2020.

Kabla ya uchaguzi, Mheshimiwa Sengo Isiaka Mtandikile – Naibu Meya aliyemaliza muda wake alijiuzuru. Aidha aliwashukuru Waheshimiwa Madiwani na Watendaji



kwa ushirikiano waliompa kwa kipindi chote cha mwaka 2018/2019.

### **Utaratibu wa uchaguzi**

Ilielezwa kuwa mshindi anatakiwa apate zaidi ya nusu ya kura zitakazopigwa. Aidha wagombea wote wataulizwa maswali kama yapo na Wajumbe. Pia wagombea walipewa muda wa dakika tatu kujieleza na kuomba kura kwa Wajumbe.

Baada ya utaratibu huo kutangazwa, Wajumbe walipiga kura za siri na matokeo yalikuwa kama ifuatavyo:-

- Waliopiga kura 39
- Kura zilizoharibika 0
- Mheshimiwa Scolastica W. Mkude alipata kura 5
- Mheshimiwa Sengo Isiaka Mtandikile alipata kura 34

Mkurugenzi wa Manispaa (Katibu) kwa mamlaka aliyopewa alimtangaza Mheshimiwa Sengo Isiaka Mtandikile kuwa Naibu Meya wa Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, Wagombea wote wawili walipewa fursa za kuwashukuru wapiga kura.

HMM/BM/4/  
2019/2020  
Kuteua  
Wajumbe wa  
kamati za  
kudumu za  
Halmashauri  
kwa mwaka  
wa fedha  
2019/2020

Kwa mamlaka waliyopewa, Mstahiki Meya na Mkurugenzi wa Manispaa waliunda Kamati za kudumu na Kamati nyinginezo kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha demokrasia ilitumika katika kuwachagua Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Huduma za Uchumi, Elimu na Afya na Mwenyekiti wa Kamati ya Mipangomiji na Mazingira.

### **MUUNDO WA KAMATI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

#### **1. KAMATI YA FEDHA NA UONGOZI.**

<b>NA.</b>	<b>JINA KAMILI</b>	<b>NAFASI</b>
1)	Mhe. Pascal M. Kihanga	Mstahiki Meya – Mwenyekiti
2)	Mhe. Sengo Isiaka Mtandikile	Naibu Meya – Mjumbe
3)	Mhe. Abdulaziz Mohamed (MB)	Mjumbe
4)	Mhe. Ally Rashid Kalungwana	Mjumbe
5)	Mhe. Spear Komanya	Mjumbe
6)	Mhe. Amiri Juma Nondo	Mjumbe
7)	Mhe. Peter Joel Dhahabu	Mjumbe
8)	Mhe. Scolastica W. Mkude	Mjumbe
9)	Mhe. Zamoyoni J. Abdallah	Mjumbe
10)	Mhe. Tunda Amini Abdallah	Mjumbe
11)	Mhe. Dismas W. Makanjira	Mjumbe

**2. KAMATI YA HUDUMA ZA UCHUMI, ELIMU NA AFYA:**

<b>NA.</b>	<b>JINA KAMILI</b>	<b>NAFASI</b>
1	Mhe. Spear Komanya	Mwenyekiti
2	Mhe. Pascal M. Kihanga	Mstahiki Meya – Mjumbe
3	Mhe. Abdul Aziz Mohamed (Mb)	Mjumbe
4	Mhe. Devotha Minja (Mb)	Mjumbe
5	Mhe. Maringo Hassan Madadi	Mjumbe
6	Mhe. Msasa M. Hamisi	Mjumbe
7	Mhe. Zawadi M. Kidando	Mjumbe
8	Mhe. Tembo Juma Abdul	Mjumbe
9	Mhe. Mizambwa R. Lugonzo	Mjumbe
10	Mhe. Milikiel M. Mahiku	Mjumbe
11	Mhe. Amina H. Zihuye	Mjumbe
12	Mhe. Madaraka S. Bidiyanguze	Mjumbe
13	Mhe. Suzana Mtikwa	Mjumbe
14	Mhe. Kuluthum Isack Mwisongo	Mjumbe
15	Mhe. Rashid Matessa	Mjumbe
16	Mhe. Zinduna Kombo	Mjumbe
17	Mhe. Castroy C. Ndulu	Mjumbe
18	Mhe. Scolastica Mkude	Mjumbe
19	Mhe. Daud Salum Mnadi	Mjumbe
20	Mhe. Samwel Msuya	Mjumbe
21	Mhe. Gabriel Temba	Mjumbe

**3. KAMATI YA MIPANGOMIJI NA MAZINGIRA:**

<b>NA.</b>	<b>JINA KAMILI</b>	<b>NAFASI</b>
1)	Mhe. Ally Rashid Kalungwana	Mwenyekiti
2)	Mhe. Pascal M. Kihanga	Mstahiki Meya – Mjumbe
3)	Mhe. Dr. Christine Ishengoma (Mb)	Mjumbe
4)	Mhe. Amiri Juma Nondo	Mjumbe
5)	Mhe. Dorothy John Mwamsiku	Mjumbe
6)	Mhe. Hilda Benedict John	Mjumbe
7)	Mhe. Dismas Winfred Makanjira	Mjumbe
8)	Mhe. Zamoyoni Juma Abdallah	Mjumbe
9)	Mhe. Peter Joel Dhahabu	Mjumbe
10)	Mhe. Nuru Majikata	Mjumbe
11)	Mhe. Mabula R. Lusewa	Mjumbe
12)	Mhe. Wenslaus Kalogeries	Mjumbe
13)	Mhe. Kifimbo Suddi Jumanne	Mjumbe
14)	Mhe. Warda Omary Baziha	Mjumbe
15)	Mhe. Gilbert Barnabas Mtafani	Mjumbe
16)	Mhe. Latifa Said Ganzel	Mjumbe
17)	Mhe. Hamisi A. Kilongo	Mjumbe
18)	Mhe. Hadija Kombo Kibati	Mjumbe
19)	Mhe. Zahara Kitima	Mjumbe
20)	Mhe. Tunda Amin Abdallah	Mjumbe
21)	Mhe. Mudhihiri Shoo	Mjumbe

**4. KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI:**

NA.	JINA KAMILI	NAFASI
1)	Mhe. Sengo Isiaka Mtandikile	Mwenyekiti
2)	Mhe. Pascal M. Kihanga	Mjumbe
3)	Mhe. Abdulaziz Mohamed (Mb)	Mjumbe
4)	Mhe. Devotha Minja (Mb)	Mjumbe
5)	Mhe. Dr. Christine Ishengoma (Mb)	Mjumbe
6)	Mhe. Daud Salum Mnadi	Mjumbe
7)	Mhe. Rashid Matessa	Mjumbe
8)	Mhe. Kuruthum I. Mwisongo	Mjumbe
9)	Mhe. Latifa Ganzeli	Mjumbe

**5. KAMATI YA MAADILI:**

NA.	JINA KAMILI	NAFASI
1)	Mhe. Madaraka Bidyanguze	Mwenyekiti
2)	Mhe. Hassan Maringo Madadi	Mjumbe
3)	Mhe. Hamisi Msasa	Mjumbe
4)	Mhe. Zawadi Kidando	Mjumbe
5)	Mhe. Mizambwa R. Lugonzo	Mjumbe

**6. KAMATI NDOGO YA MAZINGIRA**

NA.	JINA KAMILI	NAFASI
1)	Mhe Hamis Kilongo	Mwenyekiti
2)	Mhe. Mabula R. Lusewa	Mjumbe
3)	Mhe. Zahara Kitima	Mjumbe
4)	Mhe. Mudhihiri Shoo	Mjumbe
5)	Mhe. Hilda Benedict John	Mjumbe
6)	Mhe. Kifimbo S.Jumanne	Mjumbe
7)	Mhe Ally Kalungwana	Mjumbe

**7. KAMATI YA KUGAWA ARDHI:**

NA.	JINA KAMILI	NAFASI
1)	Mhe. Doroth John Mwamsiku	Mjumbe
2)	Mhe. Daudi Salumu Mnadi	Mjumbe

**8. MJUMBE WA MKUTANO MKUU WA AGM MSAMVU PROPERTIES:**

NA.	JINA KAMILI	NAFASI
1)	Mhe. Pascal M. Kihanga	Mstahiki Meya
2)	Mhe. Milkiel Mansuet Mahiku	Mjumbe

9. MFUKO WA JIMBO:

NA.	JINA KAMILI	NAFASI
1)	Mhe. Abdul Aziz Mohamed	Mwenyekiti
2)	Mhe. Milkiel Mansuet Mahiku	Mjumbe
3)	Mhe. Suzana Mtikwa	Mjumbe

10. ALAT MKOA

NA.	JINA KAMILI	NAFASI
1)	Mhe. Pascal M. Kihanga	Mstahiki Meya
2)	Mhe. Gilbert Barnabas Mtafani	Mjumbe
3)	Mhe. Warda Bazia	Mjumbe
4)	Mhe. Abdulaziz Mohamed (Mb)	Mjumbe

11. BODI YA AJIRA

NA.	JINA KAMILI	NAFASI
1)	Mhe. Amina Zihuye	Mjumbe

12. BODI YA MORUWASA

NA	JINA KAMILI	NAFASI
1)	Mhe. Hadija Kombo Kibati	<b>Mjumbe</b>

13. BODI YA NGOZI

NA	JINA KAMILI	NAFASI
1)	Mhe. Madaraka Bidiyanguze	<b>Mjumbe</b>

HMM/BM/5/  
2019/2020  
Kupitisha  
Ratiba ya  
Mikutano ya  
Halmashauri  
na Kamati za  
Kudumu kwa  
mwaka wa  
fedha  
2019/2020

Baraza la Madiwani lilipitisha ratiba ya mikutano ya Halmashauri na Kamati za kudumu kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kama ifuatavyo:-

**RATIBA YA VIKAO VYA BARAZA LA MADIWANI, KAMATI ZA KUDUMU NA KAMATI NYINGINEZO KWA KIPINDI  
CHA JULAI, 2019 HADI JUNI, 2020**

NA.	KAMATI	2019						2020					
		JUL	AUG	SEP	OKT	NOV	DES	JAN	FEB	MACHI	APR	MEI	JUNI
1	Fedha na Uongozi	25 Ziara 25 Kikao	15	16	16 Ziara 17 Kikao	14	16	15 ziara 16 kikao	13	16	20 ziara 21 kikao	14	15
2	Huduma za Uchumi, Elimu na Afya	22 Ziara 22 Kikao			7 Ziara 8 Kikao			6 ziara 7 kikao			8 ziara 9 kikao		
3	Mipangomiji na Mazingira	23 Ziara 23 Kikao			9 Ziara 10 Kikao			8 ziara 19 kikao			14 ziara 15 kikao		
4	Kudhibiti UKIMWI	24 Ziara 24 Kikao			15 Ziara 15 Kikao			13 ziara 14 kikao			16 ziara 17 kikao		
5	Maadili ya Madiwani	26			21			22			22		
6	Bodi ya Huduma za Afya	19			22			17			23		
7	Uwasilishaji wa taarifa za Kata (Madiwani)	29			29			28			28		
8	Kamati za Vyama Madiwani	30			30			29			29		
9	Baraza la Madiwani	31			31			30			30		30
10	*Kamati ya Ushauri Wilaya												
11	Kamati ya Wataalamu wa Halmashauri	4	9	11	3	11	10	3	10	10	3	11	9
12	Baraza la Wafanyakazi					28							29
13	Bodi ya Zabuni	10			18			9			17		

\* NB: Maandalizi hufanywa na ofisi ya Mkuu wa Wilaya

**RATIBA YA VIKAO VYA KAMATI NDOGO KWA KIPINDI CHA JULAI, 2019 HADI JUNI, 2020**

NA.	KAMATI	2019						2020					
		JUL	AUG	SEP	OKT	NOV	DES	JAN	FEB	MACHI	APR	MEI	JUNI
1	Vibali vya Ujenzi	5ziara 6kikao 18ziara 19kikao	5ziara 6kikao 20ziara 21kikao	4ziara 5kikao 19ziara 20kikao	1ziara 2kikao 22ziara 23kikao	4kikao 5ziara 21kikao 22ziara	5ziara 6kikao 23ziara 24kikao	2ziara 3kikao 20ziara 21kikao	5ziara 6kikao 20ziara 21kikao	5ziara 6kikao 19ziara 20kikao	6ziara 7kikao 23ziara 24kikao	8ziara 9kikao 21ziara 22kikao	4ziara 5kikao 18ziara 19kikao
2	* Kugawa Ardhi												
3	Uongozi wa Mradi wa Upimaji Viwanja 4,000												
4	Leseni za Vileo			16						16			
5	Kudhibiti UKIMWI mahali pa kazi	5			4			10			10		
6	Watumishi wote wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro	26						31					
7	Kamati ya Nyumba	30			28			31			27		
8	*Bodi ya Ajira	*5			*7			*27			*6		
9	Kamati ya Ukaguzi	10			11			10			13		
10	Kamati Ndogo ya Mazingira	22 Ziara 22 Kikao			4 ziara 4 kikao			2 ziara 3 kikao			3 ziara 6 kikao		
11	Kamati ya Mikopo ya Wilaya	25			24			23			24		
12	Kamati ya Lishe	24			29			24			20		
13*	Mfuko wa Jimbo												

\* NB: Hukutana pale tu inapotokea shughuli ya kufanya

HMM/BM/6/  
2019/2020  
Taarifa ya  
utendaji kazi  
za  
Halmashauri  
kwa mwaka  
2018/2019.

Taarifa ya utendaji kazi ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2018/2019 iliwasilishwa , ilipokelewa na Baraza liliridhia taarifa hiyo kama ilivyowasilishwa.

HMM/BM/7/  
2019/2020  
Kufunga  
Mkutano.

Mstahiki Meya aliwashukuru Wajumbe kwa ushirikiano wao. Aliomba ushirikiano huo uendelee ili Halmashauri iweze kutekeleza miradi ya maendeleo kama vile kitega uchumi cha DDC ambacho kimeombewa mkopo katika Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa jumla **Tshs. 620,000,000.00** pamoja na kufuatilia mradi wa machinjio ya kisasa.

Baada ya maelezo hayo Mstahiki Meya alifunga mkutano saa 9:10 alasiri.

Muhtasari umethibitishwa tarehe .....

.....  
Mhe. Pascal M. Kihanga  
Mstahiki Meya  
**MWENYEKITI**

.....  
Ndg. John K. Mgalula  
Mkurugenzi Wa Manispaa  
**KATIBU**

**YATOKANAYO NA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 02/11/2018**
